

IDARA YA AFYA YA VERMONT BODI YA HUDUMA YA AFYA
108 Cherry Street - PO Box 70 Burlington, VT 05402-0070
Simu: 802-6574220 / Faksi: 802-657-4227
Simu isiyolipishwa ndani ya Vermont: 800-745-7371
Barua pepe: AHS.VDHMedicalBoard@vermont.gov

IDHINI YA KUTOA REKODI ZA KIMATIBABU

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA:

NINAKUPA IDHINI upe Idara ya Afya ya Vermont, Bodi ya Huduma ya Afya, na/au mwakilishi wake mteule, na kwa Ofisi wa Mwanasheria Mkuu, rekodi zote za kimatibabu na taarifa zote, bila kusita, unazomiliki au unazodhibiti kuhusiana na **mtoto** wangu, iwe kwa mdomo au maandishi (ikiwa ni pamoja na rekodi zilizotolewa kwako na wataalamu wengine wa afya au taasisi za huduma ya afya) kuhusiana na ugonjwa au jeraha au tatizo lolote la kimiwili, kitabia, kiakili au kihisia ambalo ulitoa ushauri au huduma.

Kuhusiana tu na idhini hii mahususi ya ufichuzi kwa Idara ya Afya ya Vermont, Bodi ya Huduma ya Afya na kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, na sio kwa kusudi lingine, kwa uwazi **NINAONDOA** usiri na/au mapendeleo au ulinzi uliotolewa kwa taarifa hizi na sheria ya Jimbo au Shirikisho, ikiwa ni pamoja na nyenzo zinazojumuishwa chini ya sheria ya 42 CFR, Kifungu cha 2, na nitakuchukulia bila hatia utakapo fichua taarifa hizi kwa Idara ya Afya ya Vermont, Bodi ya Huduma ya Afya, kulingana na ombi langu, ili kutathmmini vipengele fulani vya huduma ya afya iliyotolewa kwa **mtoto** wangu.

IDHINI HII inaweza kubatilishwa wakati wowote isipokuwa kwa upeo ambao tayari umechukua hatua kwa kuitegemea. Ikiwa hajabatilishwa hapo awali, idhini hii itaacha kutumika baada ya hatua ya mwisho, ikiwa ni pamoja na uamuzi wa mahakama, kwa hatua yoyote iliyochukuliwa na Bodi ya Huduma ya Afya inayohusiana na taarifa hizi, au, ikiwa hatua kama hiyo hajachukuliwa, itaacha kufanya kazi siku 365 kutoka tarehe iliyotajwa.

UMEIDHINISHWA PIA kuripoti taarifa, iwe kwa mdomo au maandishi, moja kwa moja kwa Idara ya Afya ya Vermont, Bodi ya Huduma ya Afya, au mwakilishi wake mteule, na kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa msingi unaocendelea hadi idhini hii ibatilishwe au muda wake uishe.

CHAPA YA NAKALA SAHIHI YA IDHINI HII ITATUMIKA BADALA YAKE.

Jina la Mtoto (Andika)

Tarehe ya Kuzaliwa

Jina la Mzazi/Mlezi (Lililoandikwa)

Mzazi/Mlezi (Saini) / Tarehe

Anwani ya Barua